SHULE YA SEKONDARI LYAHIRA,

S.L.P 346 **KIDATU,**

Barua pepe: williamray.rw@gmail.com

Mobile no. 0714410818

Tarehe 15/12/2020

**Kumb. Na.** LSS/FI/2021/.........

Jina la Mwanafunzi..........................................................................................

..................................................................................................................

S.L.P.........................................................................................................

**YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LYAHIRA WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Lyahira ipo umbali wa km 129 kaskazini/mashariki/magharibi/kusini mji Mkuu wa mkoa/Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

Usafiri wa basi kutoka mjini...................................................unapatikana katika kituo cha mabasi cha ............................Nauli ni Tsh...................................Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

a)Sare ya shule hii ni Shati 2 nyeupe na Suruari 2 nyeusi kwa wavulana na Sketi 2 nyeusi na shati 2 nyeupe kwa wasichana(taja rangi na idadi).Maelezo ya mshono Linda box (ambatanisha kipande cha kitambaa).Pamoja na T-shirt ya kijivukwa wavulana na T-shirt ya kijivu kwa wasichana.

b)Rangi ya Hijab ifanane na Sare za shule(ambatanisha mshono)

c)Sare ya michezo kwa shule ni Truck suit nyeusi na T-shirt ya blue kwa Wavulana(taja rangi na idadi) na Truck suit nyeusi na T-shirt ya blue kwa Wasichana (taja rangi na idadi).

2.2 Daftari, Kalamu na Mkebe wa hesabu, Fagio,Ndoo,Jembe lenye mpini.

2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.4 Nauli ya wanafunzi wa bweni kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo,godoro na vifaa vya malazi.

2.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu(kama yapo yatajwe)

Scanned with CamScanner

3.0 Sheria na Kanuni za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji wa Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni;

a)Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation);

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

f)Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule,

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

i)Kutunza mali za umma.

3.2 )Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamiswa Shule

a)Wizi b)Uasherati na ushoga. c) Ubakaji. d)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

e) Kupigana au kupiga. f)Kuharibu kwa makusudi mali za umma.g)Kudharau Bendera ya Taifa. h) Kuwa mjamzito/kupata mimba. i)Kuoa au Kuolewa. j)Kutoa mimba.kj)Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu. l) Kukataa adhabu kwa makusudi. m)Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine Muhimu yanayopaswa Kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.b)Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.c)Fomu ya mzazi kukiri kukabiliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

RAYMOND R. WILLIAM

**MKUU WA SHULE.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI LYAHIRA
S.L.P 346, KIDATU

15/12/2020

Scanned with CamScanner

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE PRESIDENT OFFICE'**
**REGION ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITY**

## STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE.

(To be completed by government Medical Officer and returned to the Headmaster/Headmistress of Lyahira Secondary School Box 346 Kidatu-KILOSA DISTRICT)

TO THE MEDICAL OFFICER

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

RE..........................................................................................................

Please examine the above mentioned and comment on her/his health by responding to categories given below.

Thanks

.................................................... ..................................

HEADMASTER DATE

1. PREGINANCY TEST

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

2. ANY OTHER PHYSICAL DISABILITY AND COMMENTS

.............................................................................................................

.............................................................................................................

.............................................................................................................

............................................... ..........................................................

DATE NAME AND SIGNATURE (MEDICAL OFFICER)

Scanned with CamScanner

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

**SHULE YA SEKONDARI LYAHIRA**

Karatasi hii ikishajazwa irudishwe shuleni siku mtoto anapofika shuleni.
SEHEMU A:(Ijazwe na mwanafunzi)

Mimi……………………………………………………………………………………………nimesoma na kuelewa kabisa masharti yote na sheria za shule na nayakubali/siyakubali kwa hiyo naipokea/sitaipokea nafasi hiyo.(kata isiyohusika)
Naahidi kuwa nitazingatia masharti na sheria zote za shule na nitakuwa mtiifu.

Sahihi ya mwanafunzi……………………………………………………. Tarehe………………………………

SEHEMU B: (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)
Mimi Mzazi/Mlezi wake nathibitisha kuwa mwanangu…………………………………………………
……………………………………………………………………………………… na mimi mwenyewe tumeelewa maagizo,masharti na sheria zote za shule.TUNAAHIDI KUZIFUATA.

……………………………………………………… ………………………………………

Jina na sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe.

Scanned with CamScanner